SUMAIT University Journal (SUJ)
eissn (2953-2698)
Issue No. 18 June 2026

# MIKTADHA YA KAULI ZINAZOJENGA TASWIRA YA DUNIA NA UHUSIANO WAKE NA JAMII: MIFANOKUTOKA RIWAYA YA *DUNIA UWANJA WA FUJO*

*Ali Makame Mdungi*
*alimdungi395@gmail. com*
*Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni*
*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)*

*Received: Octobre 2025, Accepted: December 2025, Published: June 2026*
*© SUMAIT University Journal 20226*

**Abstract:**

*This article has examined the contexts used in expressions that construct the image of the world in the novel Dunia Uwanja wa Fujo written by Kezilahabi. The article has aimed at analyzing contexts raised in the expressions used by the writer in constructing the world image in the novel Dunia Uwanja wa Fujo with relationships obtained in those contexts and real social environment. The research results have revealed that, there are different contexts applied in the expressions that construct the image of the world in novel Dunia Uwanja wa Fujo. Among the contexts found are political context, social context, economic context, ideological or faith-based context, heroic context, counseling and romantic context. The data of this article were collected by using the library research method in which the selected novel involved and its data were picked up. Interview and group discussion methods were another methods used in collecting data of this article. The article has applied the Reader-Response theory focussing on its aspect that deals with the contexts of the text through its principle relating to contexts of the text and how they afford to be related and separated by the reader. Likewise, the article has then provided a summary of the novel Dunia Uwanja wa Fujo, explained the importances of the article together with recommendations provided by the writer of this article according to the research conducted about contexts concerned.*

***Iksiri*: *Makala hii imechunguza miktadha iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo ya Kezilahabi. Lengo lake kuu ni kufafanua miktadha iliyojitokeza katika kauli zilizotumiwa na mwandishi kujenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo pamoja na uhusiano iliyojitokeza baina ya miktadha hiyo na mazingira halisi ya jamii. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba kuna miktadha mbalimbali iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo. Miongoni mwa miktadha hiyo ni muktadha wa kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiitikadi au kiimani, muktadha wa kijasiri, muktadha wa kupeana nasaha na muktadha wa kimapenzi. Data za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya*

*udurusu matini ambapo riwaya teule ilidurusiwa na data zake zilidondolewa. Pia, mbinu ya mahojiano na majadiliano ya kundi lengwa zilitumika kukusanyia data za makala hii. Utafiti huu umetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji kupitia mhimili wake unaohusu miktadha ya matini na namna inavyoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji. Vile vile, makala imeelezea muhutasari wa riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo, umuhimu wa makala hii pamoja na mapendekezo yaliyotolewa na mtafiti kutokana na utafiti uliofanywa juu ya miktadha husika.*

**Keywords:** ***Muktadha, kauli, taswira, dunia na jamii***

## 1.0 Utangulizi

Dhana ya muktadha ni pana sana na ndiyo maana kuna wataalamu kadhaa ambao wameitolea fasili katika maandiko mbalimbali kutegemea na mahali, wakati na matendo yanayotendwa. Miongoni mwa wataalamu hao ni (1), (7), (11), (14) na (16). Neno muktadha linarejelea hali ambayo matendo huwa yanafanyika ambapo huhusisha wakati na mahali. Pia, huhusisha hali ya kimaumbile, hisi, akili na kipaji cha mtambaji pamoja na muundo wa sanaa inayotendwa ikijumuisha mada husika, hadhira, mandhari na wakati wa kufanyika na baada ya matukio hayo, (14:16). Kwa mwelekeo huo, muktadha ni kipengele muhimu sana katika uumbaji wa kazi za kisanaa kwa vile unatoa msaada mkubwa wa utambuzi wa dhamira na ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa na mwandishi wa kazi za kifasihi.

Taswira ni miongoni mwa mbinu ya matumizi ya lugha ambayo hufanya kazi ya kujenga na kuleta mvuto fulani ndani ya kazi ya kifasihi. Mbinu hii hubeba picha zinazojengwa akilini mwa msomaji au msikilizaji wa kazi husika. (10:45) ameeleza kuwa, taswira hujengwa kutokana na matumizi ya tamathali za usemi hasa sitiari, tashibiha na ishara mbalimbali zenye kuhusu mawazo, dhana, vitu au maumbile na kadhalika. Ujenzi wa taswira ndio unaomsababisha msomaji wa kazi ya fasihi kupata fahiwati kadhaa za hisi kama kunusa, kuona, kuonja, kugusa na kusikia. Kimsingi, taswira ni picha ambazo huambatana na ishara na mwanafasihi huzijenga kwa makusudi ya kuhifadhi ujumbe na dhamira anazozituma kwenda kwa jamii fulani. Pamoja na uchunnguzi uliofanywa kuhusu matumizi ya taswira katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, imebainika kuwa yapo matumizi mengine ya taswira ambayo bado hayajachunguzwa. Miongoni mwa matumizi hayo yamebainika katika vifungu ama sentensi mahususi ambazo mwandishi wa makala hii ameviita kauli zinazojenga taswira ya dunia. Vifungu au sentensi hizo zimeitwa hivyo kwa sababu katika kuundwa kwake neno dunia halikosekani katika kila kifungu au sentensi iliyohusishwa na uchunguzi huu. Vifungu au sentensi hizo kiundani, zimekusudiwa kuonesha namna dunia inavyozungukwa na matendo tofauti ya wanadamu. Katika matendo hayo yapo yanayohusu matendo mema na maovu, maendeleo ya dunia, masuala ya nguvu za mataifa makubwa dhidi ya mataifa madogo. Pia, katika kauli hizo kuna masuala yanayohusu mambo ya uchumi, siasa, utamaduni na jamii kwa ujumla.

Watafiti na wahakiki mbalimbali wa riwaya wameichunguza riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* iliyoandikwa na mwandishi Kezilahabi. Miongoni mwa watafiti na wahakiki walioichunguza riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni (13), (3), (2) na (9).

(3), (13) na (9) wameichunguza riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kwa kujikita zaidi kwenye maudhui. (2) amechunguza kipengele cha fani kinachohusu mbinu za ujenzi wa wahusika na usawiri wa sifa zao. Uchunguzi wa Ilomo umebainisha mbinu tofauti za ujenzi wa wahusika zikiwemo za kimatendo, kimatamshi, kimazingira, uzungumzinafsiya, mazungumzo baina ya wahusika na mbinu ya uwasilishaji dhahiri. Pia, uchunguzi huo umebaini kuwa, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni mfano bora wa motifu ya dunia inayoonesha kuwa ni mahali pabaya pa kuishi, duni, pasipoaminika, sehemu yenye fujo na mateso. Ubaya wa mateso hayo unatokana na uzinzi, unyonyaji, ukahaba, kushushwa thamani kwa asasi ya ndoa, maamuzi yasiyozingatia maoni ya wengi, dharau na visasi.

(9) ametafiti kipengele cha kimaudhui na kubainisha masuala muhimu yaliyoshughulikiwa na Kezilahabi katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*. Masuala hayo yalihusu zaidi Tanzania baada ya Uhuru na mengine kwa uchache yalijikita katika utamaduni wa kijadi uliobainika katika mandhari ya shamba hususan kwa baadhi ya wahusika wakulima. Masuala ya kijadi yaliyobainishwa ni pamoja na ndoa, burudani, uchawi, mgawanyiko wa vizazi na mwelekeo wa kihafidhina wa wazazi unaopingana na mawazo ya vijana wanaoathiriwa na utamaduni wa Kimagharibi. Mambo mengine ni pamoja na suala la mapenzi na namna linavyoleta athari kwa watoto pamoja na mirathi na masuala ya kisiasa. Vile vile, kuna tukio la wahusika waliochorwa kiuhalisi na kukitwa katika mazingira halisi ya kijamii, kihistoria na athari za mazingira ya maisha yao. Halikadhalika, uchunguzi wa Mbatiah umebainisha kuwa, Kezilahabi ni mwandishi anayeonesha udhaifu uliokithiri na ukosefu wa matumaini kwa sera mpya ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo ilitolewa bila elimu kutoka ngazi ya chini hadi kwa viongozi waliokuwa wakiihubiri.

(13) amechunguza kipengele cha maudhui katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na kubaini kuwa,Kezilahabi ameshughulikia masuala mbalimbali yanayohusu matatizo ya kidunia ikiwemo migogoro ya kisiasa, matatizo na mikinzano ya kijamii, kiuchumi na kifalsafa katika jamii ya Tanzania hususan baada ya Azimio la Arusha. Pia, uchunguzi umebainisha kuwa, migogoro iliyojitokeza imeibua matatizo mbalimbali yakiwemo malezi na athari zake kijamii, mvutano baina ya mji na vijiji, nafasi ya mwanamke katika jamii, mapenzi na ndoa, mvutano baina ya wazee dhidi ya vijana, upokezi wa Azimio la Arusha na falsafa kuhusu maisha.

Waandishi na watafiti waliogusiwa wameichunguza riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* katika vipengele tofauti lakini haikuwajia kabisa kukihusisha kipengele cha miktadha iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Kipengele cha muktadha katika kazi yoyote ya kifasihi ni muhimu sana na huchukua nafasi kubwa ya kuonesha mahala, wakati, hali na utendaji wa tukio linalohusika. (1:58) anasisitiza kwamba, ni muhimu kuwa makini kuhusu muktadha ambamo matukio ya riwaya au hadithi hutendeka; na hiyo haina maana ya dhana ya kijiografia tu, bali masuala ya kijamii na

kihistoria yana nafasi yao pia. Kutokana na kutogusiwa kipengele cha miktadha iliyofanyiwa uchunuzi, mwandishi wa makala hii amepata msukumo uliomsababisha kukishughulikia kiuchunguzi kipengele hicho.

Utafiti huu umefanywa kwa lengo la kudhihirisha matumizi ya miktadha na jinsi inavyoweza kuwasilisha dhamira za waandishi wa kazi za kifasihi wanazokusudia kuzituma kwa wasomaji wao, yaani wanajamii. Aidha, makala hii imekusudia kutoa ufafanuzi wa kina juu ya mambo kadhaa yaliyofichwa na mwandishi ndani ya kauli zilizofumbata miktadha iliyofanyiwa uchunguzi. Kwa muktadha huo, umuhimu mkubwa unaopatikana katika makala hii ni kuonesha namna matumizi ya mbinu za kisanaa yalivyoweza kujenga kauli zilizobeba miktadha iliyoonesha taswira ya dunia iliyoibua dhamira na ujumbe mkubwa kwa jamii. Dhamira na ujumbe huo unabeba masuala yote yanazunguka maisha ya mwanadamu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Isitoshe, kwa upande wa wasomi, wachambuzi na watafiti wa kazi za kifasihi, makala hii itawasaidia kuongeza maarifa juu ya matumizi ya mbinu za kisanaa na kwa kiasi gani zinaweza kutumiwa na waandishi katika kuwajengea uwezo wa kufikiria masuala mbalimbali yanayohitaji kufichuliwa ndani ya kazi za kisanaa.

## 2.0 Methodolojia ya utafiti

Makala hii imetokana na utafiti uliojikita katika mkabala wa kitaamuli, kwa maana hiyo, data zake zimekusanywa na kufafanuliwa kimaelezo. Utafiti huu ulifanywa katika Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuzihusisha Wilaya zake tatu ambazo ni Wilaya ya Mjini, Wilaya ya Magharibi (**A)** na Wilaya ya Magharibi (**B**). Data za msingi za makala hii zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya udurusu matini ambapo riwaya teule ilidurusiwa na kudondolewa data zake. Vile vile, data za upili nazo zilipatikana kwa udurusu wa maandiko mbalimbali yaliyohusiana na uandishi wa makala hii huko maktabani. Mbinu nyingine iliyotumika ni mbinu ya mahojiano yaliyowahusisha wanafunzi sita wa Shahada ya Uzamivu wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibr (SUZA) na wahadhiri watatu walioteuliwa na mtafiti kutoka vyuo vikuu vitatu vilivyochaguliwa na mtafiti. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Chuo Kikuu cha Abdul-Rahman Al-Sumait na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Mbinu ya majadiliano ya kundi lengwa iliwashirikisha wanafunzi wa Shahada ya Kwanza wa fasihi ya Kiswahili ambapo tisa walitoka Chuo Kikuu cha Abdul-Rahman Al-Sumait na sita walitoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Hivyo, kutumika kwa watoa taarifa hawa, kuliufanya utafiti huu kupata data toshelevu zilizoweza kukidhi mahitaji ya uandishi timilifu wa makala hii kwa kule kupatikana kwa data zilizolingana kutoka kwa sampuli yote iliyotumika.

Makala hii imetumia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika kufafanua mbinu za kisanaa zilizotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Nadharia hii imeasisiwa na Jauss Robert wa Ujerumani katika miaka ya (1970). Nadharia inashughulikia dhima na majukumu ya msomaji katika matini kwa madhumuni ya

kubainisha wasomaji na tendo nzima la usomaji. Kinachozungumziwa hapa ni kwamba, hakuna maana sawa ya kazi fulani kwa msomaji na kuwa wasomaji huvifasiri vipengele vya kiisimu na kisanaa kwa namna mbalimbali. Mhimili unaohusu miktadha ya matini inayohusu namna miktadha ya matini inayoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji ndio ulioegemezwa katika ufafanuzi wa data za makala hii. Mhimili huo unaoeleza kuwa: kubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutenganishwa na msomaji. Matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* kuna miktadha tofauti iliyotumika katika kuzijenga kauli zilizofanyiwa uchunguzi. Miongoni mwa miktadha hiyo ni pamoja na muktadha wa kijamii, kisiasa, kiuchumi, kimapenzi, kijasiri, kimapenzi, kupeana nasaha, kikahaba, kujenga ari na bidii ya kufanya kazi na kiitikadi au kiimani.

## 3.0 Dhana ya Muktadha

Muktadha huweza kuangaliwa kutokana na kazi inayoundwa, huweza kuwa ya kitamaduni, kihistoria, kijiografia, kisaikolojia, kisiasa, kimazingira ya kijamii, kiuchumi na wakati. Muktadha ni muhimu sana katika uchanganuzi wa maandishi kwa sababu husaidia kuelewa na kutafsiri maana ya matini na huelezea mazingira, hali na mambo mengine yanayohusu matini. (15) anashadidia kuwa, muktadha ni dhana inayotumika katika kuzihakiki kazi za fasihi ili kueleza hali ya kujaribu kuliweka tukio au matukio ya kazi za fasihi katika muktadha wa kijamii, kihistoria, kijiografia, kisiasa na kiuchumi. Kwa mnasaba huo, taswira kama kipengele kimojawapo muhimu cha fani katika uandishi wa kazi za fahisi, kinaonekana kuguswa na miktadha inayotokana na matukio mbalimbali yanayojiri katika jamii. Muktadha wowote wa kazi ya kifasihi lazima ufungamane na mazingira halisi ya tendo linalotendwa, wakati linapofanywa, pahali linapofanyika, muundo wa sanaa inayotendwa, dhamira, hali ya uwasilishaji pamoja na upokewaji wake. Hivyo, makala hii imefafanu miktadha iliyojitokeza katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* pamoja na uhusiano uliokuwepo baina ya miktadha hiyo na jamii zetu.

## 4.0 Muhutasari wa Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*

Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ni riwaya dhati iliyoandikwa na Kezilahabi (1975). Riwaya hii inasawiri maisha ya wanajamii wanaoishi Afrika Mashariki hususan katika nchi ya Tanzania. Ni riwaya inayoeleza maisha ya duniani kuwa ni sawa na fujo tu kwani kila mtu hudhihiri duniani na fujo zake na baadae hutoweka. Mwandishi Euphrase Kezilahabi anaeleza kuwa, fujo zinazofanywa na watu hapa duniani, hatimae husababisha matatizo mbambali katika jamii wanayoishi.

Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* inasimulia kisa cha maisha ya Tumaini mhusika mkuu, aliyekulia katika maisha ya utajiri pamoja na kuengwaengwa na wazazi wake. Pia, riwaya hii inaweka wazi maisha ya wazazi wa Tumaini pamoja na tabia ya mhusika huyu kijijini Bugolola. Kijiji hiki kimehodhi umasikini, ushirikina, visasi, umoja na vituko

anavyovishuhudia Tumaini kabla ya kuhamia mjini ambako anakumbana na ulimwengu tofauti na ule aliouzoea.

*Dunia Uwanja wa Fujo* ni riwaya inayoonesha jinsi maisha ya Tumaini yanavyoingiliana na wahusika wengine na namna yanavyokumbwa na mabadiliko ya kijamii na kisiasa. Sio tu riwaya hii, inayoonesha jinsi msako wa furaha maishani unavyoweza kusokotwa na kila aina ya vikwazo lakini pia na namna suala la malezi lilivyo changamano katika jamii ya leo. Halikadhalika, riwaya hii inazungumzia kuhusu maamuzi ya Tumaini kuhama Bugolola yeye na Anastasia kwenda Mwanza na rafiki yake John, kuhama Mwanza kwenda Jijini Dar es Salaam na safari ya kwenda kujiimarisha zaidi kimaisha alipoelekea huko Shinyanga.
Hata hivyo, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* inaonesha kwamba, katikati ya maisha yaliyokuwa na mafanikio ya wananchi pamoja na Tumaini, Azimio la Arusha likihubiri Ujamaa na Kujitegemea lilitangazwa. Kutangazwa kwa Azimio la Arusha kulileta mtafaruku mkubwa uliotengeneza machafuko yanayotokana na kutaifishwa kwa mashamba ya wananchi likiwemo shamba la Tumaini. Kutokana na tukio hilo, Tumaini anaamua kumuua Mkuu wa Wilaya ambapo hatimaye anakamatwa na kuhukumiwa kunyongwa.

Inaonekana kwamba, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imeandikwa kwa kufuata mkondo wa kiteti kwa sababu unatetea na kusuta kuhusu kufanikiwa sera ya Ujamaa iwapo ingetekelezwa ipasavyo.
Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* inabainisha ukosefu wa taaluma ambayo ilistahiki kutolewa mwanzo kabla ya kutangazwa na kuenezwa sera hii ya Ujamaa na Kujitegemea kwa watu na anaelekeza lawama zake kwenye sera mpya ya kiuchumi ya ujamaa na kujitegemea pasina kutolewa taaluma yoyote kwa watu wa ngazi ya chini na kwa hata wale viongozi walioandaliwa kuihubiri sera yenyewe.

Kwa ujumla, riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imeshughulikia matatizo na mikinzano mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutaduni na kifalsafa. Matatizo na mikinzano hiyo imeibua migogoro iliyosababisha kuibuka kwa dhamira mbalimbali zikiwemo za malezi, mvutano baina ya miji na vijiji, nafasi ya mwanamke katika jamii, mapenzi na ndoa, mvutano baina ya vizazi, upokezi wa Azimio la Arusha na falsafa kuhusu maisha. (13:83) analitilia mkazo jambo hili kwa kueleza kuwa, katika riwaya hii Kezilahabi ameshughulikia migogoro, matatizo na mikinzano ya kijamii, kiuchumi na kifalsafa katika jamii ya Tanzania hususan baada ya Azimio la Arusha. Riwaya hii ilichaguliwa na mtafiti kufanyiwa uchunguzi kwa sababu imeonesha mawanda mapana yaliyotosheleza data zilizohusiana na mada iliyoteuliwa na mtafiti kufanyiwa uchunguzi.

## 5.0 Miktadha Iliyotumika Katika Kauli Zinazojenga Taswira ya Dunia Kwenye Riwaya

**ya *Dunia Uwanja wa Fujo***

Matukio katika kauli zinazojenga taswira ya dunia ndani ya riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, yamejengwa na Kezilahabi kwa kuvishwa miktadha inayoonesha utendaji na utendekaji wa matukio mbalmbali. Jambo hili linaonesha kwamba, kila muktadha huwa na wakati, mazingira au hali ambapo matukio huwa yanatendeka, na ndiyo maana tunaona kuwa, kazi yoyote ya fasihi huwa imefungamana na muktadha maalumu. Uchunguzi uliofanywa ulibaini kuwepo miktadha mingi iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia ndani ya riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Miongoni mwa miktadha iliyotumika ni muktadha wa kiimani au kiitikadi, muktadha wa kijamii, muktadha katika uhusiano wa kimapenzi, muktadha katika kupeana nasaha, muktadha wa kijasiri, muktadha wa kiuchumi, muktadha wa kilimbwende, muktadha katika hali ya kisiasa na kiwakati, muktadha katika hali inayojenga ari na bidii ya kufanya kazi.

### 5.1 Muktadha wa Kijamii

Muktadha wa kijamii unahusu mazingira ya kijamii ambayo mtu hukulia na kuishi nayo na huwa na ushawishi unatoa maoni na tabia za wanajamii hao. Jamii ni mkusanyiko wa watu wanaoishi kwa pamoja katika eneo moja la kijiografia wakiunganishwa na historia yao na wakitambuliwa kwa utamaduni wao, lugha yao mila na desturi zao. Ili mkusanyiko fulani uweze kuitwa jamii ni lazima pawepo na watu wa jinsia na rika zote, wanaoishi pamoja katika kijiji ama mji fulani wenye eneo na mipaka maalumu. Muktadha wa kijamii unabainishwa na mwandishi kupitia wahusika anaowavisha kauli zinazodhihirisha matendo, tabia na hulka zinazohusishwa na wanajamii wa dunia halisi. Mwandishi Kezilahabi ameutumia muktadha huu katika jamii ya Bugolola lakini mshabaha wake unakwenda pia katika jamii mbalimbali za Tanzania, Afrika Mashariki na kwengineko duniani. Kezilahabi anatumia mbinu ya utomeaji kupitia Tumaini aliyekuwa akisoma kitabu kimoja miongoni mwa vitabu alivyovinunua na kuikuta kauli inayosema: *''Ulimwengu wa leo ni ulimwengu wa wanadamu kufahamiana zaidi: Mambo haya yaliumbwa na Mwenyezi Mungu ilimradi mwanadamu apate furaha hapa duniani.''* (5:16).

Kauli hii inazungumzia muktadha wa kijamii unaohimiza watu waishi katika maisha yanayotawaliwa na maelewano ya watu katika jamii. Dunia ya leo, wanajamii wote wanaishi kwa pamoja kwa kutendeana mema yaani kusaidiana, kushirikiana katika furaha na msiba na kuacha kutendeana maovu na kulipizana visasi. Kimsingi, tuzingatie kwamba, mambo haya yameletwa na Mwenyezi Mungu kwa maana ya kumtaka kila mwanadamu aishi kwa raha katika maisha yake yote hapa duniani na siyo kupata shida. Kwa upande mwingine, kauli hii inaonesha muktadha wa kijamii ambao unatilia mkazo zaidi juu ya maelewano ya mtu na jamaa yake wa karibu. Hivyo, watu wenye ufahamiano wa karibu ndio wanaopeana fursa zaidi ili waweze kuishi kwa raha zaidi hapa duniani. Jambo hili linamaanisha kwamba wanaofaidika zaidi na fursa ni wale waliokaribu na wanaopewa jukumu la kuzigawa fursa hizo kwa wahusika katika jamii. Hivyo, kutokana na mwelekeo wa Tumaini, kauli hii inaonesha maelewano yanayojikita katika masuala ya watu kukubaliana kimapenzi. Dunia ya

leo inawataka watu waache kuiogopa miili yao na waitumiye katika mambo ya kupeana raha za dunia tu na kujistarehesha kimwili.
Muktadha wa kijamii umejenga uhusiano mkubwa na mazingira halisi ya jamii kwa vile umejihusisha na matendo, tabia na hulka za wanadamu katika jamii. Muktadha huu umejikita katika kuwahimiza wanajamii kuishi katika maisha yaliyojengwa kwa misingi ya uelewano inayohusisha mambo yanayojitokeza katika harakati za maisha ya mwanadamu ya kila siku. Harakati hizo ni kama vile wanajamii kuwa na maelewano mazuri, iwe kati ya mtu na mtu, mtu na jamaa zake wa karibu, mtu na wanajamii, wanajamii kwa wanajamii na mahusiano mema yanayotokana masuala ya kupendana, kushirikiana, kusaidiana na kutofanyiana maovu. Kwa mtazamo huu, muktadha wa kijamii umeonekana kuwa na uhusiano wa kutosha na mazingira halisi ya jamii kwa vile umefungamana na mambo yenye uhusiano na jamii kama uchunguzi huu ulivyobainisha.

## 5.2 Muktadha wa Kiitikadi au Kiimani

Dhana ya itikadi inahusishwa kwa kiasi kikubwa na mwanafalsafa wa Ufaransa Destutt de Tracy ambaye aliibuni dhana yenyewe katika miaka ya (1790) kwa maana ya ‘sayansi ya mawazo, (15:41). Dhana hii imepanuliwa kimaana na huweza kutumiwa kurejelea, si tu nadharia za matabaka, bali pia maeneo mengine yanayohusisha kuwepo kwa mahusiano yasiyokuwa na haki au yanayokiuka haki. Maeneo yanayohusishwa zaidi na hali ya utabaka ni pamoja na uana au jinsia na rangi. Kwa msingi huo, ndio maana dhana ya itikadi imekuwa mojawapo ya dhana ambazo si rahisi kuzifasili sio tu kwa vile inaendana na dhana ya imani lakini pia hata ikisimama peke yake.
Itikadi ni mfumo wa mawazo fulani ambayo ni msingi wa mwelekeo fulani wa kiuchumi au kisiasa na kwamba hivyo ndivyo ilivyo (4:192). Jilala anaendelea kusema kuwa, ni mawazo yanayochukuliwa na watu kadhaa na unaweza kusema kwamba mtu fulani binafsi ana itikadi yake. (15:41) anaeleza kuwa, katika mazungumzo ya kila siku ya fasihi, itikadi hutazamwa kama mawazo au mwongozo wa kimawazo unaoudhibiti mkabala wa mwandishi kuhusiana na masuala mbalimbali. Hapa itikadi inafungwa kwa mtunzi au mwandishi wa kazi ya kifasihi. (7:173) amefafanua kuwa, itikadi ni mawazo au imani zinazofanywa na kurithishwa na jamii ambazo hazitokani na uhalisi au ukweli, mawazo au dhana hizo huathiri mielekeo ya wanajamii kuhusu lugha yao, lugha za watu wengine na hasa uhusiano kati ya jamii mbalimbali. Kwa mnasaba wa fasili hizi, dhana ya itikadi inachukua mitazamo tofauti na kukosa kusimama katika hali moja na ndiyo maana inabeba masuala mengi kama vile imani ya kidini, itikadi za kijamii, uchumi na siasa.

Katika makala hii, itikadi inachukuliwa kuwa ni mtazamo unaomsaidia mtu kusimamia imani ya kidini au mambo yanayomzunguka katika jamii yake pamoja na msimamo thabiti kuhusu utekelezaji wa kadhia hizo. Dini yaani imani, inayohusiana na mambo ya kiroho baina ya binadamu na Mwenyezi Mungu; pia ni njia mahususi ya kiumbe kuhusiana na Mwenyezi

Mungu kwa kumuheshimu na kumcha na kumtumikia, apate hatimaye kufikia heri ya milele (12: 280).

Muktadha wa kiimani au kiitikadi unapatikana katika kauli inayosema kuwa: "*Walikuwa na raha kwa sababu walifahamu kwamba maisha huwasumbua wale watu watafutao heri hapa duniani*" (5:4). Kauli hii inajenga taswira inayoonesha pande tatu: kwanza, kuna taswira inayoashiria watu wanaohangaika kutafuta maisha ya raha hapa duniani bila kufikiria maisha mengine baada ya kuondoka duniani. Maisha ya watu hawa kugubikwa na starehe za dunia na hawajali kufanya mambo ya heri kama vile kuwasaidia wasio na uwezo wa kujikimu kimaisha. Wanajiona kuwa hawahusiki katika kutenda mema na jambo hili linawahusu wale tu wanaohitajia heri itakayokamilisha amani yao mbele ya Mwenyeenzi Mungu huko ahera.

Pili, ni taswira inayoashiria watu wasioshughulishwa na maisha ya starehe hapa duniani badala yake hushughulishwa na masuala mengine yanayohusu maisha bora baada ya kuondoka hapa duniani. Watu hawa hupata shida sana ya kutafuta mambo ya heri na husumbuka sana kuona wanashindwa kutekeleza shida za watu wasiojikimu kimaisha. Hivyo, muktadha wa kiitikadi hapa unajitokeza katika hali inayoonesha kwamba, katika dunia hii wapo waumini wenye itikadi kuwa heri kamili iko kwa Mwenyezi Mungu huko ahera. Hapa duniani yapo mambo ya heri mengi tu lakini ukamilifu wake unapatikana baada ya maisha ya hapa duniani na kuanza maisha mengine mapya huko ahera. Tatu, kuna taswira inayoashiria watu waliotosheka na hali ya maisha ya dhiki waliyokuwa nayo, fikra za maisha ya raha hazipo kwao. Roho zao zimeshakinai shida na taabu zinazowasokota, watu hawa ni watu wenye bidii ya kujitafutia maisha yao tu na kuyakabili mazingira yote yanayowazunguka. Miili yao imeshazoea shida za kiangazi, kipupwe na maradhi lakini pia wakati wa neema ya mavuno mashambani wapo kufurahia.

Kwa ujumla, muktadha huu umepatikana katika kauli iliyofafanuliwa hapo juu ambapo umejikita katika pande mbili: itikadi ya kidini inayojiegemeza na maisha ya ahera na itikadi inayohusu maisha ya hapa duniani tu. Tumeona upande wa watu wanaoshughulishwa na kutafuta maisha ya milele huko ahera na wale wanaojishughulisha na maisha mafupi na ya mpito ya hapa duniani. Muktadha wa kiimani au kiitikadi umeonesha uhusiano mkubwa baina yake na mazingira halisi ya jamii kama ulivyotumika kuijenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Uhusiano huo umetokana na sababu kwamba, wanajamii duniani ndio wenye misimamo ya kutosha juu ya matendo yao ambayo huegemezwa kwenye imani na itikadi walizojiwekea ziwaongoze katika maisha ya kila siku. Wapo watu wenye kujenga imani na itikadi zao katika misingi iliyoelekezwa kwa Mwenyezi Mungu Mmoja kwenye matendo ya heri za huko ahera. Halikadhalika, wapo watu ambao imani zao zimejengwa katika misingi ya kutafuta maisha bora hapa duniani na wengine itikati au imani zao hujengwa katika utoshelevu wa kukubaliana na ile hali ya maisha inayowakabili maishani mwake.

### 5.3 Muktadha wa Kimapenzi

Muktadha huu unajitokeza kwa mhusika mkuu Tumaini ambaye anaonekana kujenga tabia ya kuwapenda wasichana tokea akiwa shuleni. Tabia hii ameianza wakati akiwa shule ya sekondari ambapo mazungumzo yake akiwa pamoja na marafiki zake katika matembezi au hata akiwa Bwenini yalikuwa yanahusu msimamo wake juu ya mapenzi kwa wasichana. Mawazo yake yalijikita katika imani kwamba, katika dunia hii hakuna mwanamme ambaye hapendi wasichana na wala hatokei wa kumdanganya. Hali hii inamsababisha kutamka kauli inayopatikana katika (5:13) inayosema kwamba:

> "Tumaini alianza kujenga mawazo kuhusu wanawake alipokuwa katika Shule ya Sekondari. Utamsikia mara nyingi akiwambia rafiki zake bwenini au matembezini: 'Hakuna mtu anayeweza kunidanganya kwamba yeye hapendi wasichana. Kusema haki wasichana ndio wanaoleta raha hapa duniani. Ukifinya chuchu zao, ukiwashika matako au kuwagusa mashavuni, utasikia mwili mzima unasisimka. Oh! Sauti zao! Mwendo wao! Namna yao ya kucheka na kurembua macho! Kweli wasichana ni maua ya ulimwengu, shibe ya macho."

Kauli hii inajenga taswira ya hisi ambayo inaashiria namna mtu anavyopata raha na burudani ya moyo akiwa anatembea na wasichana kimapenzi. Pia, kauli hii inajenga taswira inayoonesha kuwa mwanamke ni chombo cha starehe kinachotumiwa na mwanamme kumfurahisha, kumstarehesha na kumliwaza nafsini mwake kama inavyodhihirika kwa Tumaini kutokana na kujisikia raha wakati anapowashika wanawake sehemu za miili yao. Tumaini anaathiriwa na jambo hili kwa kiasi kikubwa na kumsababisha kuzama katika masuala ya kusoma hadithi na vitabu vingine vinavyohusu mapenzi na kusahau vile alivyotakiwa kuvisoma ambavyo vinalingana na kuendana na masomo yake. Tumaini ni kijana aliyerithi fedha nyingi kutoka kwa wazazi wake hivyo alikuwa na uwezo wa kununua kitu chochote alichokihitaji maishani mwake. Kutokana na hali hiyo, Tumaini, kwa vile alikuwa tayari ameshaathirika na kuwapenda wasichana kimapenzi, alikuwa na uwezo wa kutumia fedha zake nyingi kuwavuta wasichana hususan wenye tabia ya kupenda fedha. Hivyo, mhusika huyu anajenga taswira inayowasawiri watu katika jamii ambao wanaamini kwamba wanaume wote wanapenda kufanya mapenzi na wasichana na hakuna kitakachowadanganya kuwa kuna mwanamme ambaye hapendi kustarehe na wanawake. Watu hawa hutumia fedha nyingi katika masuala ya mapenzi na wakati mwingine wanasahau utekelezaji wa majukumu muhimu ya maisha yao.

Kutokana na ufafanuzi uliofanywa na mtafiti, muktadha huu umebainika kujenga uhusiano imara na mazingira halisi ya jamii kwa sababu suala la mapenzi linatawala katika mfumo

mzima wa maisha ya mwanadamu. Suala la mapenzi kwa binadamu na viumbe hai wengine halina kizuizi, hujitokeza siku na wakati wowote, muhimu ni makubaliano yanayoweza kuliruhusu kuanza. Mapenzi hayaangalii rangi, kabila au taifa, hujiingiza katika rika zote hususan rika la vijana, kama wanavyowakilishwa na Tumaini, hushamiri zaidi. Kundi kubwa la wanajamii limejaa mawazo kwamba wanawake wameumbwa kwa ajili ya kuwaburudisha, kuwastarehesha, kuwaliwaza na kuwafurahisha kimapenzi wanaume. Kwa msingi huo, muktadha wa kimapenzi uliojitokeza katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, umejenga uhusiano adhimu na mazingira halisi ya wanadamu ndani ya jamii zetu.

### 5.4 Muktadha wa Kupeana Nasaha

Kauli inayojenga muktadha wa kupeana nasaha ameitoa mhusika Dennis; kwa rafiki yake Tumaini wakiwa katika mazungumzo ya kubadilishana mawazo kuhusiana na uhalisi wa maisha. Mawazo ya Dennis yamehusiana na dhana ya "*Dunia Uwanja wa Fujo"* ukizingatia namna anavyomnasihi rafiki yake Tumaini. Watu wanaposema kuwa Dunia uwanja wa fujo hawana maana ya kuandaliana vita, ugomvi, kuibiana, kuchinjana, kunyang'anyana thamani wanazomiliki, watu kuwa walevi, wazinzi na wauwaji. Dunia uwanja wa fujo maana yake ni kuishi kwa kuvishinda vikwazo vinavyoyakwaza maisha bora na kujenga nia ya kufikia maendeleo endelevu. Dennis anasema hivi:

> "Hapa lazima tuelewane," Dennis alisema. "Niliposema kwamba *Dunia uwanja wa fujo* sikuwa na maana kwamba ni kawaida na ni lazima watu kuchinjana au kupigana. Jambo ninalotaka kusema ni hili: kama tunataka kuishi vizuri, lazima tukubali taabu hizi kiume na tusitafute njia ya mkato ya kupata heri na furaha hapa duniani." (5:65)

Kulingana na kauli hii ya Dennis, watu hawapaswi kabisa kujitafutia maisha kwa njia ya mkato, yaani kutengeneza maisha kwa kujihusisha na vitendo vya utapeli, kuwapora watu mali zao na kujihusisha na biashara haramu kama kuuza dawa za kulevya. Maisha mazuri yenye heri na furaha hapa duniani yanahitaji bidii na uvumilivu wa vikwazo vyote vitakavyokukabili wakati wa harakati za kujitafutia maisha mazuri. Ukiwa masikini unatakiwa apambane ili ujikwamuwe katika vikwazo vya umasikini, hutakiwi kuupa nafasi umasikini.

Ijapokuwa Dennis na Tumaini ni wahusika katika ulimwengu wa kubuni wa Kezilahabi, lakini wameumbwa kuwa wawakilishi wa matendo yanayofanywa na wanadamu katika ulimwengu halisi. Kupeana nasaha ni jambo la wajibu kwa wanadamu wote duniani kwani nasaha huweza kujitokeza katika hali tofauti kama vile kunasihiyana katika kuhimizana, kuongozana, kukosoana, kuzinduana, kuelekezana, kuonyana na kutanabahishana. Kupeana nasaha huwafikisha watu kwenye masuluhisho ya matatizo mbalimbali yanayowavaa katika maisha yao ya kila siku. Muktadha huu unatupa nasaha kwamba tunatakiwa kupambana sana katika kujitafutia maisha bora hapa duniani na tujiepushe na vitendo viovu kama vile, wizi, utapeli, uzinzi na ukahaba, kuua na kufanya biashara haramu. Pia, tunanasihiwa kwamba

tusipende kujitafutia maisha kwa njia ya mkato badala yake tufanye kazi kwa bidii, uvumilivu, nidhamu na kuchunga mipaka ya haki tukiwa kazini. Kwa mantiki hii, muktadha wa kupena nasaha una uhusiano mkubwa na maisha halisi ya jamii. Jambo hili linatokana na sababu kwamba, wanajamii ndio wanaopaswa kujikaza kiume, kufanya kazi kwa bidii, kuwa wavumilivu wakati wa kufanya kazi na wasikubali kutafuta maisha bora kwa njia ya mkato.

### 5.5 Muktadha wa Kijasiri

Muktadha huu umejitokeza katika kauli iliyojikita kwenye mazungumzo ya Dennis na rafiki yake Tumaini. Tumaini anamtanabahisha Dennis kwamba, maisha wanayoishi hawako peke yao bali wapo watu wengine duniani ambao wanaishi maisha ya ujasiri kama tunavyoishi sisi. Aidha, mhusika huyu anamzindua Dennis ili kuvuta umakini wa kuelewa kwamba, katika kadhia hii hawako peke yao, wapo watu wengine ambao wamejitolea muhanga na wamejiandaa vyema kupambana na maisha kwa ujasiri mkubwa, hivyo wanafanana na sisi. Pia, watu hawa wameamua kikamilifu kupambana na vigingi vinavyozuia mtu kufikia maisha bora kama tunavyopambana sisi. Kwa kuwa watu kama sisi wapo, hao ni majasiri na bila shaka wameweza kugeuza maisha yao kutoka hali dhaifu na kupanda juu kwenye matumaini ya kujenga maisha bora hapa duniani. Tumaini na Dennis wanaonekana kuwa ni vijana imara walioonesha ujasiri mkubwa kwa vile wameweze kujikomboa kimaisha. Kutokana na kufanya kazi kwa bidii na uvumilivu Dennis na Tumaini wanaokana kuishi katika maisha bora pamoja na familia zao, wameshinda nguvu ambazo zingevunja harakati za kujenga maisha bora na yenye fahari hapa duniani. Hivyo, vijana hawa wameonesha ujasiri mkubwa duniani kwa kujiimarisha kiuchumi na wamesahau hali duni walizotoka nazo kijijini kwao Bugolela.

Vijana hawa walitambua kwamba, kwa hakika maisha bora duniani hutafutwa kwa kufanya kazi zenye uzalishaji unaoleta tija zinazoweza kukidhi mahitaji muhimu ya maisha ya kila siku. Maisha hayapatikani bure bure, lazima kuwe na kazi za uhakika na zisiwe za kubahatisha, ifanane kama Tumaini alivyoamua kujiegemeza kwenye kilimo kilichohusisha pamba ambalo ni zao la biasha. Mtu jasiri ni yule anayeweza kusimama imara, kumiliki uwezo wa kukabili maisha ya kila siku, kuchapa kazi kwa bidii, kujiwekea misingi imara ya uzalishaji na uhakika wa kuvishinda vikwazo vinavyodumaza maisha mazuri hapa duniani. Katika muktadha huu wa ujasiri, Kezilaahabi anasema:

> “Dennis,” Tumaini alisema, kati ya watu waishio hapa duniani sisi hatuko peke yetu. Kuna watu wengi kama sisi ulimwenguni. Lakini ni watu wangapi ambao wamekata shauri kama sisi tulivyokata, shauri ambalo lingeweza kuyageuza maisha yao?” (5:112)

Kauli hii kama ilivyofafanuliwa hapo juu, imejenga muktadha wenye taswira inayowaonesha watu ambao wamo katika harakati za mapambano ya kujitafutia maisha bora hapa duniani kwa kujenga nidhamu ya kuchapa kazi kwa ujasiri mkubwa. Watu hawa wanaonekana kuvumilia shida zinazowakabili kwa kujikaza kiume kufanya kazi, lengo ni kupata maisha yenye kuridhisha. Katika harakati za kupambana na ukali wa maisha, vikwazo mbalimbali hujitokeza. Hivyo, watu wenye moyo wa ujasiri wa kujenga maisha bora na ya halali kama Dennis na Tumaini, huvishinda vikwazo na utaratibu wa harakati za maisha huendelea inavyostahiki.

Muktadha huu wa ujasiri unaowaonesha Dennis na rafiki yake Tumaini wakiwa katika maisha ya matumaini wao na familia zao, umetiwa nguvu na kauli nyingine ya Dennis inayoonesha kuwa siku zote mwanzo wa kufanya jambo lolote lile unakuwa mgumu. Kadri siku zinavyoendelea, ndivyo hali hiyo inavyozoeleka na hatima yake huonekana kuwaa ni ya kawaida. Kwa vile, Tumaini na Dennis ijapokuwa walikuwa wameshaanza kuonja ladha ya maisha ya matumaini, bado walijiona kuwa ni wapya katika shughuli za kutafuta maisha bora duniani. Watu wanaopenda kujituma kufanya kazi kama Tumaini na Dennis wamekubaliana na hali zote ngumu zilizowasokota katika upya wao wa mapambano ya kujenga uchumi imara wa maisha yao. Maisha duniani ni fujo, fujo hizi zinatokana na zile harakati mbalimbali za maisha kama vile kufanya biashara, kutafuta elimu, kushiriki katika shughuli za kilimo, kufanya ibada na kusafiri. Hivyo, Dennis na Tumaini walipenda kuishi katika fujo za dunia za kufanya kazi kwa ari na ujasiri. Tumaini kwanza, aliajiriwa kuwa usala wa taifa lakini kutokana na matatizo aliyoyapata kwa kujeruhiwa na watu wabaya, kazi hiyo aliiacha na baadae alijiingiza katika shughuli za kilimo. Dennis yeye aliajiriwa kuwa usala wa taifa.

> "Ndivyo nasi tulivyo. Huu unaweza ukawa ni mwanzo tu wa taabu mpya. Hivyo ndivyo ulimwengu ulivyo – uwanja wa fujo. Na katika fujo hii sisi twapenda kuishi." (uk:113)

Kwa hivyo, kauli hii nayo imechukua nafasi ya kubeba muktadha unaoonesha ujasiri wa kukubaliana na mazingira ya upya wa kufanya kazi kwa matumaini kwamba hali hiyo ni ya mpito na baada ya muda si mrefu hali za wanaohusika zitakubaliana nayo. Isitoshe, wanadamu duniani wanatakiwa wakubaliane na fujo za dunia kwani kujishughulisha nazo ndiyo mfumo mzima wa maisha duniani.

Muktadha huu unaifunza jamii kuwa na bidii na ujasiri mkubwa katika kupambana na vikwazo vinavyoweza kukatisha tama katika harakati za kujenga maisha bora hapa duniani. Kila mtu anatakiwa kufanya kazi kwa bidii, kukubali taabu zote zitakazo mkabili na kujiepusha na mawazo yanayoweza kumpotosha na kumkatisha tamaa katika kupambana na kujiinua na kujiendeleza kimaisha. Kila mtu katika jamii anatakiwa kukubaliana na ugumu unaojitokeza mwanzo wa kufanya kazi kwa hiyo ni hali ya kawaida na baada ya hapo

huondoka. Kufungamana na hali ya ujasiri, humjenga mtu katika maisha bora na ya heri hapa duniani ambayo humwezesha kujitegemea kwa kutumia mbinu zinazofaa na hujiepusha na mbinu za kujipatia kipato kwa njia ya mkato. Muktadha wa ujasiri umebeba uhusiano mkubwa na mazingira halisi ya jamii kwa kuhimiza watu kuwa na ujasiri wa kutekeleza majukumu ya masuala mbalimbali yanayowakabili katika maisha yao ya kila siku. Uhusiano huo umetokana na sababu kwamba, kila mmoja katika jamii duniani anatakiwa kuamini kuwa hayuko peke yake katika kujishughulisha na harakati za kuhangaikia maisha bora. Kuna watu wengi katika jamii ambao kila mmoja ameamua kujiletea maendeleo yanayoweza kuyabadilisha maisha yake kutoka kwenye hali duni na kufikia hali bora kabisa. Ujasiri hujenga bidii, ari na maarifa yanayomfikisha mtu katika maendeleo ya maisha yake binafsi na taifa kwa ujumla. Zaidi ya hayo yote, muktadha wa ujasiri unachukuwa nafasi kuifunza jamii kuwa, fujo za duniani ni jambo lisiloweza kuepukika kilaa mmoja duniani anawajibu wa kufanya kazi kwa lengo la kukamilisha utu wake na maisha mazuri kwa ujumla.

## 5.6 Muktadha wa Ukahaba

Ukahaba huelezewa kuwa ni biashara ya mapenzi (ngono) na mara nyingi hujadiliwa katika muktadha wa kijamii, kisheria au kielimu. Ukahaba ni kitendo au hali ya mtu hasa mwanamke, ijapokuwa na wanaume wapo, kuuza au kutoa huduma za ngono kwa malipo ambayo mara nyingi huwa ya fedha au vitu vingine vya thamani. Ukahaba hutazamwa kama ubaya unaovunja heshima hasa wanawake, yaani malaya. Mtendaji anayepokea malipo huitwa kahaba, changudoa au malaya na washiriki wanaotoa malipo huitwa wateja. Muktadha wa ukahaba unajitokeza kwenye kauli inayopatikana katika kipande cha habari kutoka gazeti moja la nchini Tanzania, kupitia mhusika Mama Resi akiwa nyumbani kwake. Kauli hiyo imenasibishwa na ukahaba kwa sababu wanadamu wamekuwa huru katika matendo maovu kama vile kutoiogopa miili yao, kuiuza na kushiriki katika matendo ya ngono kwa uhuru mkubwa.

> “Hakuna mjinga duniani kuliko mtu anayeogopa mwili wake mwenyewe au mwili wa mtu mwingine. … Katika nchi hizi madaktari wanaojifunza tabia na matendo ya binadamu wamevumbua kwamba mwanadamu anaweza kupata furaha kubwa hapa duniani kwa kutumia mwili wake.” (5:74)

Kauli hii inajenga muktadha unaodhihirisha picha inayoashiria harakati za watu kuuza miili yao, kutembea utupu na kuhalalisha masuala ya ngono. Muktadha huu pia unaashiria namna watu hususan wa zile nchi za Kimagharibi ambako utamaduni na sheria zao zinawapa uhuru kuitumia miili yao watakavyo wenyewe. Vile vile, kauli inajenga muktadha wenye picha inayoashiria kuwa, katika nchi hizo mtu mwenye kuhifadhi mwili wake kwa kujistiri vizuri kimavazi na asiyejihusisha na masuala ya ngono kuwa mjinga, anayeogopa, asiyeuthamini mwili wake, na bado hajaendelea. Miongoni mwa sababu zinazowajenga tabia hizo ni

matokeo ya tafiti zao za kitaalamu zinazohusu tabia na matendo ya binadamu kugundua kuwa, furaha kubwa ya mwanadamu hapa duniani inaweza kupatikana kwa mtu kutumia mwili wake.

Ni ukweli usiopingika kwamba miongoni mwa furaha kubwa anazozipata mwanadamu ni kujistarehesha kimwili iwapo atakuwa haki ya kisheria na uwezo mzuri unaomwezesha kulifanya tendo hilo la kimahusiano. Lakini inampasa mwanadamu kuelewa kwamba hilo ni jambo kubwa na la kiheshima lililowekewa mipaka, kanuni na sheria zake, na wala si haki kuzichupa kanuni na sheria hizo. Dini na tamaduni za wanadamu zinawataka wafuasi wao walitekeleze jambo hilo kwa utaratibu wake na kwa kuzingatia nidhamu na mipaka yake.

Muktadha wa ukahaba umejitokeza kutokana na kudhihirika kwa masuala ya ngono yanayofanywa katika nchi zilizoendelea au nchi za Kimagharibi kwa kuhusisha watu wa rika zote. Watu hawa wameonekana kutembea katika hali ya utupu na kuuza miili yao ili kupata fedha za kutimiza mahitaji ya maisha yao ya kila siku. Tumeona kwamba sheria na tamaduni za nchi za Kimagharibi zinawaruhusu watu wake kushiriki katika masuala ya ngono na ukahaba. Matendo haya yametambaa hadi kujiingiza katika nchi za dunia ya tatu na watu wake wameyapokea kwa kuyakumbatia na wameyashiriki kikamilifu. Kwa namna hiyo, kutakuwa na uhusiano wa moja kwa moja baina ya muktadha wa ukahaba na jamii zetu. Jambo hili limesababishwa na kukithiri matendo ya ngono na ukahaba, watu kujiuza miili yao na hata wanathubutu kufanya kitendo kiovu kabisa cha ndoa za jinsia moja bila hofu wala woga wa aina yoyote. Mambo haya yote yanafanywa na watu katika mazingira halisi ya jamii zetu.

### 5.7 Muktadha wa Kiuchumi

Muktadha wa kiuchumi umejitokeza wakati mwanasiasa kutoka Dar es Salaam alipowahutubia wananchi wa Mjini Shinyanga. Alihutubia katika mkutano uliohusu Azimio la Arusha linalohusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na Vijiji vya Ujamaa. Muktadha wa kiuchumi unawasilishwa na kauli inayosema:

> Nitawaambia siri moja. Na siri hii muizingatie: *Dunia uwanja wa fujo;* ndiyo, Dunia uwanja wa fujo. Sizungumzii fujo ya machafuko kama vita, ugomvi, mauaji n. k. Ninazungumzia fujo ya kiuchumi. Kiuchumi duniani kuna fujo kali" (5:117).

Kauli hii imejenga muktadha unaoashiria mapambano na mvutano wa kiuchumi katika mataifa yote duniani na namna yanavyohangaika kutafuta mbinu za kujenga uchumi imara katika mataifa yao. Kila taifa linaonekana kujivinjari na kuhakikisha linafikia katika hatua ya juu ya maendeleo kiuchumi. Hivyo, fujo za kiuchumi zinazokusudiwa hapa ni zile zinazoonekana katika taswira inayoashiria masuala yanayohusu uchumi wa dunia ambapo kila taifa linajitahidi kujinasua na vikwazo mbalimbali vinavyoudumaza uchumi wake. Kwa mfano, kuna vikwazo vya misaada na mikopo yenye masharti magumu, vinavyowekwa na

mataifa makubwa dhidi ya mataifa madogo ambayo ndio yenye uchumi duni duniani. Kikwazo kingine kinasababishwa na soko la dunia kushusha bei bidhaa za mataifa masikini kwa makusudi ya kuzididimiza kiuchumi nchi hizo. Vile vile, fujo za kiuchumi duniani zinasababishwa na mataifa makubwa kuziwekea vikwazo nchi zisizokubaliana na matakwa yao, huweza kuwa mataifa makubwa kwa makubwa na pia mataifa madogo duniani. Zaidi ya hapo, fujo za kiuchumi duniani zinadumazwa na vita visivyomalizika kwa baadhi ya nchi au vinavyoibuka baada ya nchi fulani kutofahamiana kidiplomasia na nchi nyingine au mataifa kwa mataifa au hata vita vya wenyewe kwa wenyewe ndani ya nchi.

Tanzania kwa wakati huo, ilipambana na fujo za kiuchumi kwa kuanzisha sera mpya ya Ujamaa na Kujitegemea, kutangaza Azimio la Arusha na kutaifisha mali za wananchi kama vile makampuni, majumba, mashamba na mabenki. Hivyo, Tanzania nayo ikashiriki kikamilifu katika kufanya fujo za kiuchumi duniani kwa kuanzisha Vijiji vya Ujamaa, na kutaifisha mali za wananchi ili kumiliki uchumi wa nchi.
Muktadha wa kiuchumi umejenga uhusiano na mazingira halisi ya jamii duniani kwa vile mataifa yote duniani yamo katika harakati za kujenga na kuimarisha uchumi wa nchi zao. Kila taifa linapambana kutafuta mbinu muwafaka za kukuza na kuimarisha uchumi wake kwa lengo la kufikia hatua ya juu kiuchumi wenye kuleta maendeleo endelevu. Kutokana na hatua hiyo, muktadha huu umeonesha kuwa na uhusiano mkubwa na mazingira halisi ya jamii duniani kwa kuwa kila taifa linajitahidi kutafuta mbinu za kujenga uchumi imara unaoliwezesha kuepukana na vikwazo vinavyoweza kusababishwa na mikopo yenye masharti magumu.

## 5.8 Muktadha wa Kisiasa

Muktadha wa kisiasa umejitokeza wakati ambapo wananchi wa mjini Shinyanga walikuwa na hamu kubwa ya kutaka kujua mwanasiasa, muheshimiwa kutoka Dar es Salaam, amekuja na ujumbe gani kutoka serikalini. Mheshimiwa alizungumzia misingi miwili ya Ujamaa: usawa wa binadamu na suala la unyonyaji hususan katika kufanya kazi. Kila mtu anatakiwa kuafanya kazi isiwe kuna wengine wasiopenda kufanya kazi na kuishi kwa nguvu za wengine. Pia, kuna unyonyaji mwingine unaohusu kumiliki mashamba mengi na makubwa na wengine hawana, wanalima kwa kuwalipa wamiliki wa mashamba hayo. Azimio la Arusha haliruhusu unyonyaji wa aina yoyote, hivyo ni makosa makubwa binadamu mmoja kumnyonya binadamu mwingine. Hivyo, waliomiliki mali nyingi serikali ilizitaifisha na wenye mashamba mengi walibakishiwa moja yaliyobakiya yaligawiwa kwa wananchi wengine.

Kauli iliyobeba muktadha wa kisiasa ilisema ifuatavyo: “Mkutano ambao hotuba aliyoitoa mwanasiasa huyo, kidogo–kama siyo sana–ilihitalifiana kimawazo na mawazo ya Dennis; hasa kuhusu *Dunia Fwanja wa fujo”* (5:120). Kauli hii inaonesha kupingana kwa mawazo ya

Dennis na yale aliyoyaeleza mwanasiasa hususan ufafanuzi wa maana ya kauli "*Dunia Uwanja wa Uujo."* Kimsingi, ufafanuzi wa mwanasiasa umejikita upande mmoja ulioshikilia fujo za dunia za kiuchumi tu kwa mataifa, taifa, jamii na kwa mtu binafsi. Dennis alimuona mwanasiasa alikuja kwa lengo la kushadidia azma ya serikali kutekeleza sera ya Ujamaa na Kujitegemea inayohimiza usawa katika kufanya kazi na kuondosha suala la unyonyaji.

Mtazamo wa Dennis, duniani kuna fujo nyingi ukiachilia mbali zile zilizofanywa kuyataifisha mashamba ya akina Tumaini, majumba na milki nyingine za wananchi, kuna fujo za ukandamizaji wa tabaka la juu dhidi ya tabaka la chini, vyombo vya dola kutumia nguvu za ziada. Halikadhalika, kuna fujo za wanajamii kuvunja mila na desturi za utamaduni wao, kuvunjiana ndoa, ugomvi usiokwisha, wizi na ujambazi. Zaidi ya hapo, duniani kuna fujo za kufanya kazi kwa bidii, kufanya biashara halali, kutafuta elemu, uvumbuzi wa mambo mapya, kufanya tafiti zinazohusu tiba za magojwa thakili na kutafuta amani na usawa wa kila binadamu duniani.

Tumaini alitekeleza kwa vitendo maana ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kwamba kila mtu atumiye akili, juhudi na maarifa yake kuhakikisha kwamba, anafanya kazi kwa bidii ili ajipatie maandeleo yake mwenyewe. Hatima ya hayo yote, Tumaini anajiona yuko katika wale wanaonyang'anywa mali zao na anashindwa kuvumilia na kufanya maamuzi mabaya sana ya kumuua Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga.

Muktadha wa kisiasa nao pia una uhusiano na mazingira halisi ya jamii kwa sababu jamii zote duniani zinaendeshwa kwa mifumo ya kiutawala, itekelezwe kwa misingi ya kidini, kimila, kibepari au kijamaa itahesabiwa kuwa ni mifumo ya siasa kwa vile unafuata nidhamu ya uongozi na wanaoongozwa. Tanzania kama taifa, liliwahi kuongozwa na mfumo wa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea iliyofuata misingi iliyohimiza watu wote waishi kwa usawa na wasiwepo wanaoishi kwa kuwanyonya wengine. Uhusiano huu pia unajitokeza kwa kuwa kuna baadhi ya wanasiasa hutumia nguvu za madaraka yao kuwapora watu mali zao au hutafuta sababu za kuzitaifisha.

### 5.9 Muktadha wa Kujenga Ari na Bidii ya Kufanya Kazi

Kazi ni sehemu ya maumbile ya mwanadamu, ndiyo maana Mwenyeezi Mungu akamuumba na viungo muhimu vitakavyoshiriki katika utendaji wa kazi zake. Viungo hivyo ni pamoja na mikono, miguu, macho, masikio na ubongo ambao unahifadhi akili ya mwanadamu. Kazi zote ni muhimu kwani zinachangia kuleta maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla. Ukosefu wa kufanya kazi ndio unaosababisha watu kusumbuka na kushindwa kumudu maisha ya kila siku, hatima yake kujihusisha na matendo maovu ya uzinzi na ukahaba, wizi na uporaji wa mali za watu. Mohamed na Vuzo (8:2) wanashadidia umuhimu wa kufanya kazi na hatima ya ukosefu wa kufanya kwa kusema kuwa:

> "Ni dhahiri kwamba mtu akikosa kazi husumbuka kwa sababu kazi ni uti wa mgongo wa mwanadamu, yaani: hata kama mtu ana uwezo wa kuyamudu maisha yake, bado huhitaji kufanya kazi kwani akifanya hivyo, husikia raha moyoni mwake."

Kauli inayosema kuwa, **"**Lakini nitakukumbusha. Ulisema kwamba *Dunia Uwanja wa Fujo,* kwamba kila mtu lazima atumie kichwa chake ajitahidi, afanye kazi kwa bidii ili apate kujiendeleza" (5:129). Kauli hii inajenga taswira inayoashiria watu wanaofanya kazi kwa juhudi kubwa, akili na maarifa ili wajikomboe katika hali duni za maisha duniani.

Hii ni kauli ya Dennis anakumbushwa na rafiki yake Tumaini ambaye yuko kifungoni jela akiisubiri siku yake ya kunyongwa. Kauli hii ilikuwa na maana nzito na ndiyo maana iliganda katika ubongo wa Tumaini kwa muda mrefu sana kiasi ambacho Dennis mwenyewe alikwisha isahau.Tumaini aliifanyia kazi kauli hii na ndiyo maana aliishughulisha akili yake katika kutafuta mbinu mwafaka zitakazomfanya kubuni miradi itakayojenga maendeleo ya maisha yake. Kwa vile Tumaini alielewa kwamba, kazi ndiyo kipimo cha utu mwema, alijifunga imara na kujivisha bidii na ari ya kufanya kazi na hatima yake alitajirika. Fujo ya Tumaini ilifanikiwa kwa kufanya kazi kwa bidii na ari kubwa inayomfikisha katika malengo yake ya kujipatia maendeleo ya kiuchumi. Kitendo cha Tumaini kunyang'anywa mali zake kinampandisha hasira kubwa, anashindwa kuvumilia na anafanya fujo ya mauwaji kwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga. Kitendo cha mauaji kwa m
ujibu wa maana ya fujo ukiachilia mbali tafsiri ile ya kisiasa, pia ni fujo miongoni mwa fujo zinazofanywa katika dunia hii.

Kwa ujumla, miktadha iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia ndani ya riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* zimeonekana kuwa na uhusiano mkubwa na mazingira halisi ya jamii. Uhusiano huo umebainika kutokana na sababu kwamba, yale yote yanayojitokeza katika ulimwengu wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kupitia kauli zilizofanyiwa uchunguzi, ni matendo yanayoonekana kutendwa na wanajmii duniani. Maisha ya mwanadamu hapa dunia yametawaliwa na fujo za aina mbalimbali zikiwemo za kufanya kazi, fujo za mataifa makubwa kuyaonea mataifa madogo, migogoro ya kila siku katika jamii, vita vya wenyewe kwa wenyewe, ugomvi wa nchi na nchi, mataifa kwa mataifa au mataifa kwa taifa. Pia, tunashuhudia fujo za mtu binafsi katika kupambana na hali ya kujitafutia maendeleo yake mwenyewe na taifa lake, fujo za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Halikadhalika, kuna fujo za watu kuibiana mali, fujo za mapenzi, uzinzi na ukahaba, fujo za kutafuta elimu na fujo nyinginezo. Wafanya fujo wote hawa, kila mmoja huwepo duniani kwa muda wake maalumu na ukimaliza hujiondokea na kawaacha wengine waendeleze fujo zao hadi nao maisha yao yamalizike.
Muktadha unaojenga ari na bidii ya kufanya kazi umeonekana kujenga uhusiano na mazingira halisi ya jamii kwani kufanya kazi kwa bidii ndio mbinu kuu ya kujenga msingi

wa maisha bora hapa duniani. Kazi ni muhimu na ndiyo kipimo cha utu wa mwanadamu, huleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Ukosefu wa kujenga ari na bidii ya kufanya kazi husababisha mtu kushindwa kumudu mahitaji muhimu na ya lazima katika maisha yake ya kila siku. Watu duniani huhimizwa kujifunga imara na kufanya kazi kwa ari, bidii na uvumilivu kubwa ili wafikie kipimo cha utu na maendeleo endelevu. Kwa namna hii, muktadha wa kujenga ari na bidii ya kufanya kazi, umejenga uhusiano wa kutosha na mazingira halisi ya jamii kwa vile kila mtu duniani amewajibishwa kufanya kazi ili aweze kuishi maisha yanayostahiki. Kinyume cha kutekeleza wajibu huu, ni kushindwa kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu ya mwanadamu kuletwa duniani kwa lengo la kuiimarisha dunia kwa kutekeleza ibada ya kufanya kazi kwa bidii, ari na uvumilivu. Kufanya kazi kwa bidii ndiko kunakoifikisha dunia katika maendeleo kwenye kila sekta kama vile usafiri, kilimo, ujenzi, viwanda na elimu.

## 6.0 Mapendekezo

Makala hii imeshughulikia miktadha iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* pamoja na uhusiano wake na mazingira halisi ya jamii zetu. Muktadha ni kipengele muhimu sana katika uandishi na uchambuzi wa matini za kifasihi kwani husaidia kuleta tafsiri ya maana kamili ya matini inayohusika. Kwa kuwa muktadha hubeba mazingira, hali, wakati, mahali, utamaduni na hstoria katika maandishi ya kifasihi, uchambuzi wa kipengele hiki ueleweke kuwa ni kisaidizi kikubwa katika kutafuta maana ya matini za kifasihi. Kwa muktadha huo, makala hii imependekeza mambo kadhaa yashughulikiwe na waandishi wanaofuatia. Hii inatokana na sababu kwamba, yaliyogusiwa kwenye makala hii ni machache mno ukilinganisha na mawanda ya matumizi ya kipengele hiki cha muktadha, hususan kwenye tasnia ya riwaya ya Kiswahili. Kwanza, tafiti nyingine zinazohusu hali tofauti za kimiktadha zifanyike ili kusaidia kubainisha tafsiri za matini za kifasihi. Pili, kuna haja ya kuhusisha kazi nyingine za kifasihi kutokana na sababu kwamba uchunguzi uliofanywa umejikita katika kazi moja tu. Tatu, mbali na kuuhusisha utanzu wa riwaya, makala hii inapendekeza ufanyike uchunguzi wa kipengele hiki cha muktadha katika tanzu nyingine za fasihi andishi kama vile tamthiliya na ushairi. Nne, zaidi ya uchunguzi uliofanywa kwa kuuegemeza kwenye utanzu wa fasihi andishi, pia makala hii inapendekeza kufanyika tafiti nyingine ambazo zitajikita kwenye uchunguzi wa miktadha inayopatikana katika tanzu tofauti za fasihi simulizi ya Kiswahili.

## 7.0 Hitimisho

Makala hii imekusudia kuchunguza miktadha iliyotumika katika kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Katika kulifikia lengo hilo, makala hii imefafanua miktadha mbalimbali iliyofichwa ndani ya kauli zinazojenga taswira ya dunia

kwa lengo la kuonesha namna mwandishi wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* alivyofanikiwa katika matumizi ya kipengele cha taswira. Miktadha iliyochunguzwa kwa kweli imeakisi maisha halisi ya mwanadamu katika jamii. Aidha, kupitia miktadha hiyo, imeonekana kuwa maisha ya ulimwengu wa ubunifu uliosawiriwa katika riwaya teule yameweza kuakisi vyema maisha ya ulimwengu halisi wa wanadamu. Kutokana na ufafanuzi wa kina uliofanywa juu ya miktadha iliyobainishwa, imeonekana wazi kwamba kumejitokeza uhusiano mkubwa baina ya miktadha hiyo na mazingira halisi ya jamii kama ilivyooneshwa katika kila muktadha husika. Makala hii imeonesha umuhimu mkubwa katika kukisheheneza kipengele cha taswira hususan kwenye taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Tunaweza kusema kuwa taswira ni kipengele muhimu katika kazi za kifasihi kwani zinapochunguzwa kitafsiri huibuliwa maana zilizojificha ndani yake. Hivyo,mwandishi Kezilahabi amejitahidi vya kutosha kuisawiri dunia katika miktadha ilipatikana ndani ya kauli zinazojenga taswira ya dunia kwenye riwaya yake ya *Dunia Uwanja wa Fujo.* Miktadha imebainisha mambo mengi yakiwemo ya kufanya kazi kwa bidii, kupatikana ujasiri katika maisha ya kila siku, masuala yanayohusu ndoa, mapenzi, ukahaba, itikadi, kupeana nasaha, na bidii katika kufanya kazi. Mambo haya yote yanahusisha nyanja kuu zinazopatikana katika maisha ya mwanadamu kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Wito wa makala hii ni kushajiisha kwamba, uchunguzi zaidi ufanyike kuhusiana na kipengele muhimu cha taswira pamoja na miktadha inayofungamana nazo. Kufanya hivyo, kutaongeza mawanda ya vipengele viwili hivyo pamoja na kuibua dhana mbalimbali zilizofichwa na waandishi kwenye mbinu za kisanaa walizozitumia, hususan mbinu zinazoibua miktadha na taswira.

## Marejeleo

[1] Hawthorn, J. (1985), “Studying the Novel: An Introduction,” Edward Arnold – A Division of Hodder and Stoughton, London: New York, Melbourne and Auckland.

[2] Ilomo, L. F. (2015) “Mbinu za Ujenzi wa Wahusika na Usawiri wa Sifa Zao: Uhakiki wa Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* ya E. Kezilahabi” *Mulika.* Na. 34: 38-50. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

[3] Ilomo, L. F. (2014), “Dhima ya Msimulizi Katika Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo: Kiswahili*, Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Juz. 76:160-169, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

[4] Jilala, H. (2016), *Misingi ya Fasihi Linganishi Nadharia, Mbinu na Matumizi*, Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

[5] Kezilahabi, E. (2016), *Dunia Uwanja wa Fujo,* Nairobi: Vide ~ Muwa Publishers Limited, Nairobi.

[6] Kezilahabi, E. (1975), *Dunia Uwanja wa Fujo,* East African Publications, Arusha.

[7] King’ei, K. (2010), “Kuchunguza Dhamira Zinazojengwa na Taswira,” *Misingi ya Isimujamii, Taasisi ya taaluma za Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

[8] Mohamed, S. A. na Vuzo, A. C. (1999), *Stadi za Kiswahili*, Kidato cha Tatu, Nairobi: Oxford University Press.

[9] Mbatiah, M. (2016), *Riwaya ya Kiswahili:Chimbuko na Maendeleo Yake,* The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

[10] Msokile, M. (1993), *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: EAEP.

[11] Mulokozi, M. M. (2017), *Taaluma ya Lugha na Fasihi-2, Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili, Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu*, Dar es Salaam: Kauttu.

[12] Nkwera, FR. F. V. (ht), *Tamrini za Fasihi Simulizi, Sekondari na Vyuo*, Dar es Salaam: Kitabu Commercial Printing Co. Ltd.

[13] Senkoro, F. E. M. K (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU Ltd.

[14] Songoyi, E. M. (1997), *Oral Literature 1,* Faculty of Arts and Social Sciences, Dar es Salaam: The Open University of Tanzania.

[15] Wamitila, K. W. (2015), *Kanzi ya Fasihi 1*, *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide ~ Muwa Publishers Limited.

[16] Wamitila, K. W. (2004), *Kichocheo cha Fasihi, Simulizi na Andishi*, Nairobi: Focus Publications Ltd.